KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

15/= Ksh

Volume 30

5th Rabi ul-Aakhar 1434

15th Feb, 2013

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

WASIFU WA SHEIKH NASSOR BACHU NA KAULI ZA MASHEKHE WA AFRIKA YA MASHARIKI WALIOSHUHUDIA JUHUDI ZAKE KATIKA ULINGANIZI WA DA'WA YA HAKKI

MAZIKO YA SH. NASSOR BACHU

MTAFARUKU mkubwa kati ya familia na wanafunzi wa Mwanachuoni Mkubwa wa Afrika Mashariki, Nassor Abdallah Bachu aliyefariki juzi jioni huko Chukwani Mjini Zanzibar.

Mtafaruku huo umekuja baada ya wanafamilia kuchimba kaburi mbele ya kibla cha Msikiti ambayo amesaliwa huku wanafunzi wa Sheikh huyo wakisema hawezi kuzikwa katika kibla cha Msikiti kwa kuwa ni kinyume na mafundisho ya dini ya kiislamu.

Kamati ya maandalizi ya mazishi hayo imesema kitendo kilichofanywa na wanafamilia kuchimba kaburi mbele ya msikini ni kinyume na alivyokuwa akihubiri wakati wa uhai wake ambapo mara zote alikuwa akikataza waumini wa dini ya kiislamu kuzikwa ndani ya msikiti au mbele ya msikiti.

Akiongozwa kamati hiyo Sheikh Nurdin Kishki aliwatangazia waumini kuwa na subra wakati kamati ya maandalizi ya Sheikh

(Endelea Kwenye Uk. 4)

WASIFU WA SHEIKH NASSOR BACHU (رحمه الله)

NA: *THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA.*

Sheikh Nassoro Bachu ni Mzanzibari khalis aliyezaliwa katika kisiwa cha 'Unguja' katika kijiji cha "Donge Panga Mauwa" katika mwaka wa 1951 ikiwa ni Upande wa babake, na vile-vile anahusu kijiji cha "Fuoni" ambapo sasa ni ng'ambo ya mji wa Zanzibar. Katika utoto wake, Sheikh Nassor amesoma katika Shule ya Msingi ya "Kidonge Chekundu" iliyopo Zanzibar na baadae kujiunga na Shule ya "BenBela", baada ya hapo akawacha elimu ya Sekula na moja kwa moja akaegemea zaidi na masomo ya elimu ya Dini ya ki-Islamu. Akiwa hapa Zanzibar, Sheikh Nassor alijiunga na mitaala nchini Misri akiwa akitumiwa kwa posta na kufanikiwa vizuri. Mashekhe ambao alisoma kwao ni Sheikh Abdallah Saleh al -Farsy kabla kuondoka nchini Zanzibar kuelekea Mombasa, Kenya.

Sheikh wake mkubwa moja kwa moja aliyechukuwa elimu kwake ni Sheikh Sayyid Njugu ambaye darsa zake ziliogopwa sana na viongozi wa Serikali na kufikia kufungiwa katika utawala wa Rais wa awamu ya pili wa Mzee Abuod Jumbe Mwinyi.

Baadhi ya wanafunzi aliosoma nao ni kina ash-Sheikh Awesu, Sheikh Zagari, Sheikh Ali Ahmad na wengineo ambao wote wamekufa isipokuwa sheikh Ali Hamad,

Kwa mujibu wa mahojiano niliyofanya nao, Sheikh Ali Hamad amesema: "Sheikh Nassoro alianza kudarasisha katika Miskiti hapa Zanzibar ya kikwajuni na raha-leo wakati alipokufa sheikh wao Sheikh Sayyid Njugu. Wakati huo pakapigwa kura baina ya Sheikh Nassoro na Sheikh Ali Hamad yupi atachukuwa nafasi ya Sheikh kudarasisha.

Baada ya kura kwa kuona Sheikh Nassor yuko juu kuliko Sheikh Ali Hamad ndipo sheikh Nassor akachukuwa nafasi hiyo na kuanza darsa katika misikiti hiyo ambapo amedarasisha darsa zisizopunguwa 876 na kuzidi.

Sheikh Nassor alipata wakati mgumu nchini Zanzibar kwa kusimamia Sunnah na kupinga udhalimu wa serikali wakati watu walikuwa wamezowea dini ya babu zao wa Uislamu wa kurithi na akida chafu. Sheikh alianza kushika kasi hiyo kuanzia miaka ya 1980 mpaka watu wakaanza kuijuwa Sunnah ni kitu gani. Kufika mwaka wa 2008, Sheikh alipatwa na maradhi ya stroke na kupelekwa hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Zanzibar na baadae kuhamishwa mpaka Hospitali kuu ya Rufaa ya Muhimbili iliyoko Jijini Dar-es Salaam. Baada ya kugundulika kichwa chake kimefanya maji, madaktari wakajitahidi kumtibu lakini wakagunduwa tatizo ni kubwa na hapo wakamuamulia kumpeleka India.

Sheikh Said Gwiji ambaye ni mmoja wa waandamizi wake wakubwa na watu wa karibu alisema yakuwa madaktari walisema sheika alipatikana akiwa na tatizo kubwa kiasi ambacho madakatri nchini india waliamua kumrudisha nyumbani.

Sheikh Nassor katika da'wah yake mjini Zanibar alikuwa ni mwenye wanafunzi wengi sana na wafuasi wengi kiasi amabacho baadhi ya masheikh wasiokuwa mrengo mmoja kushtuka sana na kuanza mikwaruzano ya hapa na pale.

Nikizungumza na Sheikh Ibrahim Alhabshy, Imaam wa Msikiti wa Jibril ameniambia yakuwa pamoja na khitilafu zilizokuwepo nchini Zanzibar juu ya msimamo wake mara nyigi walikuwa wakikaa pamoja kushauriana namna gani Waislamu watakuwa kiyu

(Endelea kwenye Uk. 2)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

kimoja bila ya kufarikiana.

Sheikh Nassoro ameuguwa mfululizo kwa muda wa miaka minne na hapo ikawa sababu ya madaktari kumzuia kusomesha kutokana na afya yake na mara kwa mara ametangaziwa kufa zaidi ya mara tatu lakini kufikia jana tarehe 13/2/2013 Sheikh akaaga dunia akiwa na umri wa miaka 62.Sheikh amekufa akiacha wake watatu na watoto wasiopunguwa 15. Sheikh alikufa jana huko "Mbweni Chukwani" nyumbani kwa kaka yake mkubwa,

Kifo cha Sheikh kimeweka huzuni kubwa nchini Zanzibar na Afrika ya Mashariki kwa vile ilikuwa hufanya ziara makhusus kutembelea kwa ajili ya Da'wah, kama vile Mombasa nchini Kenya na sehemu nyinginezo.

Mazishi yameandaliwa na umma mkubwa ukajitokea ambapo "Chukwani" kwa kakae wanawake walijaa na kumswalia baada ya hapo akaletwa msikitini kwake "Kikwajuni" ambapo wanawake tena zaidi ya elfu tano, kuanzia chini mpaka juu walijaa na kufunga njia zote za "Kikwajuni" mpaka "Maisara" na hapo pia wakamswalia.

Wanaume walikusanyika viwanja vya Mnazi mmoja ambapo watu walifurika katika sehemu mbali mbali za Zanzibar na jirani yake kama vile Mombasa nchini Kenya, Dar-es-Salaam na kisiwa cha pili cha Zanzibar ambacho ni Pemba. Mazishi hayo yalihudhuriwa na viongozi mbali mbali wa kidini na wa kisiasa huku kwa Serikali ya Zanzibar akihudhuria Makamu wa kwanza wa Rais Ma'allim Seif Sharif Hamad, na Waziri katika Ofisi ya makamu wa pili wa Rais, mheshimiwa Muhammed Abuod Muhammed na wengineo. Vile-vile kadhi Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khamis Haji, Mufti Mkuu wa Zanzibar Sheikh Swaleh Omar Ka'ab walikuwapo hapo na waandamizi wao, Mashekhe kutoka Kenya, Dar-es–Salaan na sehemu mbali mbali walihudhuria.

Nikifanya mahojiano na Kadhi Mkuu na Mufti Mkuu pamoja Dr.Issa Zidi ambaye ni Muhadhiri muandamizi katika Chuo Kikuu cha Taifa cha zanzibar SUZA wamesema wamehuzunika sana kupokea habari hizi kwani wanajuwa umuhimu na mchango mkubwa aliotowa Sheikh Nassor katika Zanzibar na Afrika ya Mashariki kwa ujumla na kuwataka Waislamu kuwa wamoja hata kama khilafu ziko.

Nikifanya mahojiano na Sheikh kishki kwa wageni kutoka Dar-es-Salaam na Abuu Qataadah kutoka Mombasa, Kenya waliojawa na huzuni pia wamesema wanaujuwa na kuuthamini mchango wa Sheikh na juhudi zake na kuwataka Waislamu wa Zanzibar na Afrika ya Mashariki kuzienzi juhudi zake. Baada ya kumaliza kuswaliwa katika viwanja vya Mnazi mmoja, msafara ukaanza kuelekea kijijini kwao "Donge panga mauwa" ambapo ni msafara sijaonapo maishani mwangu, magari yasiyopunguwa 300, hadi kufika saa tano tumewasili "Donge" ambapo tayari kaburi lilikuwa lishakwisha kuchimbwa ambapo lilisababisha mzozo mkubwa wa wana-familia na wanafunzi wa Sheikh. Wanafamilia walikuwa wamechimba kaburi mbele ya kibla cha Msikiti eti ni mtu mtukufu kwa vile azikwe na watukufu mwenzake, jambo ambalo limezuwa mtafaruku mkubwa na kubidi kaburi kufukiwa na kuchimbwa jingine. Hadi kufikia Saa Tisa dakika thelathini kaburi limemalizwa na uzikaji ukaanza. Inna lilah wa inna ilayhi

SHEIKH NASSOR BACHU
DA'I ALIYEKUWA SHUJAA, FASWAHA NA ALIYEKUWA NA KIPAWA CHA UHODARI WA KUBAINI.

NA: SH. HAMMAD M. KASSIM (KADHI MKUU MSTAAFU WA JAMUHURI YA KENYA)

Nilimuona mwisho katika mwezi wa December, 2012, nilipokwenda katika hafla ya ukumbusho wa KUMBU-KUMBU za Ma'ulamaa, kama Sheikh Abdallah Saleh al-Farsy na wengineo huko Zanzibar. Alikuwa wakati huo amepata Baridi kubwa (Stroke) na ijapokuwa alikuwa na fahamu zake, lakini hakuweza kuzungumza. Alikuwa amewekwa kwenye kiti. Aliniangalia sana lakini sikujua kama alinitambua.

Sheikh Nassor Bachu alikuwa akinijua vyema kwa sababu tumewahi kuwa pamoja mara nyingi na tumewahi kuwa pamoja kwa siku kadha katika Ramadhani ya 1998, katika ardhi tukufu ya Makkah na Madinah tulipokuwa huko kwa ualishi ma'lum. Hapo ndipo khaswa nilipojua tabia yake ya *TAWAADHU', UCHAJI MUNGU NA IKHLAAS.* Na tulikuwa tukijadili mambo tafauti tafauti. Kwahivyo hali aliyokuwa nayo December 2012, ilinisikitisha sana ikanifanya nitokwe na machozi.

Sheikh Nassor wengi wanamjua kama Sheikh ambaye aliyekuwa akihubiri UISLAMU SWAHEEH pasi na kujali lawama za mwenye kulaumu. Kipawa cha sauti yake kundufu na uhodari wake wa kubaini na kupanga maneno uliwaacha wasikizaji wake wasihisi uchofu wala wasitake Darsa yake imalizike. Alikuwa akingojwa kwa hamu killa mahali alipokuwa akienda kwa kutoa waadhi. Misikiti ilikuwa akimpigania killa mahali katika Afrika ya Mashariki ili kujivunia kutoa kwake Darsa katika Misikiti hiyo.

Ama Unguja na Pemba, umaarufu wake ulikuwa si wa Da'wah peke yake, bali ni wa kuwaongoza Ma'ulamaa' wa Sunnah ambayo Zanzibar ilipata pigo tangu kuondoka huko al-Marhum Sheikh Abdallah Saleh al-Farsy. Wanafunzi wake waliwahi kupata mtihani wa kushikwa na hata kupigwa risasi na wengineo kuuliwa walipokuwa wakitetea Hijaab na Sheriya ya Ki-Islamu. Leo ukiwa Zanzibar, ni nusra kumuona mwanamke wa Ki-Islamu ambaye hakujisitiri vizuri. Mimi naamini ni katika juhudi za bwana huyu.

Nilipokuwa kadhi wa Nairobi, nilipata mgeni anayeitwa *AISHA WANGARI MHANDO* kutoka Australia. Yeye ni Mkenya mwenye asili ya Kikikuyu na alikuwa amesilimu karibuni. Nilipokuwa nikimuuliza ni vipi alikuwa Muislamu, akaniambia kuwa alikuwa akiishi Australia na baadhi ya Waislamu ambao waliokuwa na desturi ya kusikiliza kaseti za mawaidha ya Sheikh Nassor Bachu. Baadae aliwasiliana na Sheikh Bachu mwenyewe na akapiga shahada na kuwa Muislamu.

Mimi sifikiri kuwa nina ujuzi wa kutosha wa kuyaeleza mengi ya Sheikh Nassor, lakini machache niyajuayo yatosha katika hii mistari michache. Allaah Amuweke mahala pema pamoja na wema. Aameen.

SHEIKH NASSOR BACHU: VYEO VYA WANAZUONI KATIKA MUJTAMA'

NA: ABU BILAAL ATHMAN BIN NA'MAN

Himdi zote ni zake Yeye Allaah anayestahiki kuhimidiwa na kuabudiwa kwa Hakki na Swala na Salamu zimfikie Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Aali zake na Swahaba wote.

Nin jambo lisilo na shaka kwa Muislamu yoyote juu ya cheo cha Mwanachuoni katika Uislamu. Na kwanini isiwe hivyo hali Allaah (سبحانه وتعالى) amewatukuza na kuwainua Daraja katika kitabu chake cha Qur'an, aliposema: **"Allaah atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa ilimu watapata daraja zaidi."** [al-Mujaadilah 58:11].

Na aya nyingi ndani ya Qur'an zenye kutuonyesha umuhimu na vyeo vya watu hawa mbali na mafundisho swaheeh ya Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) yaliyokuja kueleza juu ya fadhla za wanazuoni, watu ambao ni warithi wa Mitume. Walobeba risala na wakapata taabu kwa ajili ya Allaah.

Watu ambao wanaotakiwa Rehma na Maghfira na viumbe vilivyoko katika Mbingu na Ardhi, bali na hata Samaki Baharini pia kama ilivyokuja katika hadeeth swaheeh. Watu ambao tuloambiwa ndani ya Qur'an turegee kwao wakati wa shida kama ilivyo katika Surat an-Nisaa' aya ya 85, na mengi yalokuja katika Nusoos za kisheriya. Watu hawa ni Taa na Nuru katika Ummah ikizima huwa ni hasara na msiba kwao.

Mmoja miongoni mwa ma-Salaf alisema: "Kifo cha Mwanachuoni wa Sunnah ni pengo kubwa katika Mujtama' [halizibiki]. Na akasema tena mmojawapo miongoni mwa ma-Salaf: "Sheitwani ana furaha anapokufa Mwanachuoni, Mchaji Mungu na anahuzunika anapokufa Mjinga, mwenye kufanya Ibada [kwa ujinga]. Kwa Munaasaba ya maneno haya leo, Ummah wetu wa Africa ya Mashariki umepata msiba mkubwa wa kuondokewa na Da'ee mkubwa katika ma-Du'aat [walinganizi] wa Sunnah katika nchi ya Zanzibar. Naye si mwengine illa ni Sheikh Nassor Abdallah Bachu, aliyetuondokea juzi tarehe 13/2/2013 Muwaafaka na tarehe *3 Rabee-uth-Thaani, 1434. INNAA LILLAAHI WAINNAA ILAYHI RAAJI'OON.* Ewe Mola tupe Ujra katika msiba huu na utupe badala bora.

Sheikh Naasor alikuwa ni Da'ee, mwalimu mlezi katika Africa ya Mashariki hutopita katika Idhaa'a ya ki-Islamu na maduka ya kuuzwa vitabu vya dini na kanda za mawaidha illa utakuta ndani yake CD za Darsa zake, Mihaadhara, vitabu alivyokuwa akivifundisha na ziyara mbalimbali zake za ki-Da'wah alokuwa akifanya mbali na wanafunzi wake na waume tunawaona wakipeleka dawaa yote ni dalili ya kuafikiwa dawaa yake na matunda yake.

Katika historia ya Unguja tujuavyo, hatujapata kusikia wala kuona mtu alosimama akaitangaza na kuieneza dawaa' ya Sunnah Zanzibar baada ya kuondokewa na Sheikh Abdallaah Saleh a-Farsy Unguja illa Sheikh Nassor Bachu baada ya miaka mingi na juhudi aloifanya ilikuwa ni kubwa nakumbuka kabla ya miaka mitatu au minne, niliwahi kwenda na wenzangu ziyara ya ki-Da'wah Unguja na kufanya semina ya siku nne katika msikiti wake wa Michenzani na ulikuwa ni wakati alikuwa ashaanzwa na maradhi ya kusimamisha harakati nyingi zake za ki-Da'wah. Hakika alitupa moyo kwa naswaha zake juu ya kuieneza Sunnah na uvumilivu alokuwa nao ni mkubwa sana akitwambia kauli yake maarufu [asoitaka Sunnah hamtaki Mtume].

Umma wa ki-Islamu na watu wa Unguja khaswa umepatwa na msiba mkubwa. Na kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakuwa hataiondoa Ilmu, kuiondoa kwenye vifua vya Wanazuoni lakini ataiondoa 'Ilmu kwa kuwaondowa wanazuoni." [al-Bukhaari].

Alikuwa ni mtu wa Ibada pamoja na maradhi. Swala ya Jamaa' ilikuwa haimpiti, alikatazwa kutoa Darsa, lakini nyumbani kwake tumeshuhudilia *BLACK -BOARD* akisomesha watu nyumbani. Wanawake hakuwaacha nyuma. Kwa hakika ni mengi ya kusema na hatuwezi kuyamaliza, ilobaki ni kumuombea Du'aa Allaah aja'aliye 'amali zake katika Miizaan ya hasanaat zake. Alitie kaburi lake na ampe Kauli Thaabit.

INNAA LILLAAHI WAINNAA ILAYHI RAAJI'OON.

SHEIKH NASSOR BACHU: NILIVYOMJUA SHEIKH NASSOR BACHU

NA: AHMAD MUHAMMAD MSALLAM

Mimi nilivyomjua Sheikh Nassor Bachu ni kwamba alikuwa ni Mlinganizi wa Dini aliye Muadilifu. Kabla ya kukutana na ma'Ulamaa' wa Sunnah, alikuwa na baadhi ya mambo aliyoyashikilia ambayo hayakubaliwi na wana Sunnah, lakini hakuwa mzito wa kuikubali Sunnah kokote inapomfikia.

Sifa nyengine aliyokuwa nayo alikuwa akiheshimu sana *Du'aat* wenzake. Tulipokwenda Zanzibar kwa mjadala wa Mwezi na mengine aliwaambia wenzake: "Uongozi wa timu yetu na uwe ni wa wa-Kenya." Na akanitaja mimi niwe ndiye "Chairman" wa upande wetu. Hakuwa akenda nyumbani kwake illa baada ya kuhakikisha kwamba kila kitu chetu kiko sawasawa.

Alituahidi yakwamba atakuja kututembelea Kenya. Basi hakuja peke yake, alikuja na ujumbe mzima akakatisha Barnaamij zake ili apate kuhudhuria Darsa ya Masjid Tawbah niliyokuwa nimeipanga mimi. Lakini na mimi alipokuja nilikata Darsa yangu nikampa yeye nafasi ambayo aliichukuwa baada ya kumuomba sana. Na mazungumzo yake yote, na *mi'amala* yake yote yalikuwa ni ya ki-Islamu baada ya kuwa ni ya ki-binadamu. Namuomba Allaah amuweke pema peponi."

wakitawanywa baada ya kusali sana la

(Endelea Kutoka Uk. 4)

Eid El Hajj ambapo hali hiyo ilianzia wakati wa utawala wa Dk Salmin na kumalizikia kwa Rais Mstaafu Amani Karume.

(Continued from page 1)

huyo ikiwa ikifanya mazungumzo na wanafamilia ili kufikia mwafaka wa wapi lichimbwe kaburi lake, huku kila mmoja aliyekuwepo katika mkuanyiko huo wakisomeshana namna ya kuzikana maiti za kiislamu.

Wakati waumini hao wakitakiwa kuwa na subra baadhi ya waumini wamekwenda kulifukia kaburi la awali lililochimbwa na kusema haitowezekana kuzikwa katika eneo hilo na kutafutwa eneo jengine kwa ajili ya kuulaza mwili huo.

â€œWaumini tunakuombeni jamani muwe na subra lakini tunasema daima mwenyewe Marehemu Sheikh Nassor wakati wa uhai wake alikuwa akipinga suala la kuzikwa ndani ya msikiti au mbele ya msikiti lakini kaburi tunaliona limechimbwa mbele ya msikiti huku ni kwenda kinyume na mafundisho ya dini ya kiislamu na pia ni kinyume na kile alichokuwa akikihubiri na kukisomesha, hatuwezi kuwaingilia wanafamilia kwa kuwa sisi ni wanafunzi wake tu Sheikh lakini wao ndio wenye maiti na wao ndio wenye haki lakini tunawaomba sana katika hili tusende kinyume na diniâ€ alisema Kishki mbele ya umati mkubwa.

Baada ya vuta ni kuvute hizo wanafamilia waliingia ndani ya msikiti na kujifungia na hatimae kutoa tamko la kuuliza ni masafa gani ambayo wanataka likachimbwe kaburi na mwili wa marehemu ulazwe.

Akizungumza na baadhi ya waandishi wa habari, Said Masoud Gwiji ambaye ni miongoni mwa wanafunzi wake Sheikh Nassor na pia ni mwana kamati ya maandalizi ya mazishi alisema kwamba ni vizuri wana familia wakafahamu kwamba alichokuwa akikihubiri Sheikh Nassor kiendane na kile kinachotekelzewa mwisho wa uhai wake.

Alisema sio busara kuvutana lakini kwa kuwa mafundisho ya dini ya kiislamu yanakataza kaburi kuchimbwa karibu na msikiti ni vyema likazingatiwa hilo na mazishi hayo kaburi likachimbwa kando na msikiti.

Hatimae wanafamilia na wanafunzi wa Sheikh Naassor wakakubaliana kuchimba kaburi mbali na msikiti na mazishi yakafanyika huku umati mkubwa ukiwa unashuhudia huku kila mmoja akitaka kushika maiti hiyo jambo ambalo limezusha ahama kubwa kutokana na umati mkubwa.

Naye Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad ameungana na melfu ya waumini wa dini ya Kiislamu jana katika mazishi ya Mwameanachuoni na Mhadhiri Mkubwa wa Dini ya Kiislamu Zanzibar, Sheikh Nassor Abdallah Bachu amefariki dunia juzi Chukwani Mjini Unguja.

Sheikh Nassor Bachu amefariki majira ya saa 5 mchana juzi baada ya kuugua kwa muda mrefu akisumbuliwa na kiharusi ambapo alisafirishwa kwa matibabu nchini India na katika hospitali mbali mbali za Dar es Salaam na Zanzibar kabla ya kufikwa na mauti.

Mwili wa Marehemu Sheikh Nassor ulilazimika kusaliwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja kutokana na kuwa hakuna Msikiti mkubwa ambao ungeweza kuhimili maelfu hayo ya watu waliofika kwa ajili ya kushindikiza mwili huyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa ummati mkubwa kama huo kushiriki mazishi ya Mwanachuoni huyo ambapo awali alitakiwa kusaliwa katika Msikiti wa Kikwajuni aliokuwa akiendesha darsa wakati wa uhai wake lakini kutokana na umati mkubwa ilishindikana na kuamuliwa kusaliwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja, na baadae magari yamefuata msafara kuanzia Skuli ya Haile Sellasie na kuelekea Donge kwa kuzikwa ambapo kuanzia Mjini hadi Donge barabara imejaa wananchi wakisubiri njiani kuona msafara uliobeba maiti hiyo.

Mazishi ya Sheikh Nassor hayajawahi kutokea ambapo mbali ya ummati mkubwa kuja kushuhudia mazishi hayo wanawake na wanaume walioanzia Chukwani alipomalizikia uhai wake, na baadae kuletwa katika uwanja na Mnazi Mmoja na kupekelekwa huko Donge maelfu ya waumini wameonekana kusubiri maiti njiani na kushuhudia msafara mkubwa uliokuwa ukiongozwa na gari ya Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad.

Viongozi wengine waliohudhuria mazishi hayo ni pamoja na Waziri wa Ofisi ya Makamo wa Pili, Mahammed Aboud Mohammed, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khamis Haji, Katibu Mtendaji wa Wakfu na Mali ya Amani Sheikh Abdallah Talib na Masheikh mbali mbali kutoka Nairobi, Mikoa ya Tanzania Bara, na wenyeji wao Zanzibar.

Sheikh Nassor alinza kufundisha mafunzo ya dini ya Kiislamu kwa kuendesha darsa mbali mbali katika Misikiti ya Kikwajuni na Rahaleo mnamo mwaka 1978 baada ya Mwalimu wake Sheikh Said Njugu kuanza kuumwa na kushindwa kuendesha darsa hizo ambapo majina ya wanafunzi wa Sheikh huyo yalipendekezwa matatu akiwemo Sheikh Ali Ahmad, Sheikh Othman Ali na yeye Sheikh Nassor Bachu.

Mwalimu wake Sheikh Nassor pia aliwahi kupigwa marufuku kufanya mihadhara na kuendesha darsa na Mzee Aboud Jumbe Mwinyi aliyekuwa Rais wa Zanzibar wakati huo jambo ambalo linelezwa kwamba kabla ya kifo chake Sheikh Said Njugu alikwenda kuombwa radhi na Mzee Aboud Jumbe.

Wanafunzi wa mwanzo ambayo amewasomesha Sheikh Nassor alivyoanza kuendesha darsa ambapo alianzia na wanafunzi wachache akiwemo Abdulghani Msoma ambaye ni Katibu Ofisi ya Utawala Bora, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Abdallah Rashid na Ali Juma Shamhuna ambaye ni waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Sheikh Nassor Bachu alianza kuvuma katika miaka 80 ambapo alikuwa na upinzani mkubwa kati yake na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyokuwa ikiongozwa na Rais wa wakati huo Dk Salmin Amour Juma ambapo alionekana kuhimiza wajibu na maadili ya kiislamu kufuatwa jambo ambalo lilikuwa likionekana ni geni kwa wakati huo.

Mbali kupingwa na viongozi wa serikali lakini pia Sheikh Nassor alipata upinzani mkali kutoka kwa Maulamaa na Masheikh mbali mbali wa dini ya Kiislamu kutokana na kutangaza kwake msimamo wa kufuata Sunnah -Mila za Mtume Muhammad (s.a.w) ambapo waislamu walionekana kupingana naye.

Msimamo wa Sheikh Nassor Bachu ulikuwa ni kukataza kuadhimishwa kwa kuzaliwa kwa Mtume Muhammaa (s.a.w) kwa kusomwa maulid na akitaka maadhimisho hayo yawe ni kufuata matendo yake badala ya kukusanyika, pamoja na suala la muandamo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kufuatwa popote unapoonekana jambo ambalo lilikuwa likipingwa na baadhi ya Maulamaa hapa nchini wakitaka lazima Mwezi uonekane nchini na utangazwe na serikali.

Changamoto alizokumbana nazo Sheikh Nassor katika uhai wake ni nyingi ikiwemo kutengwa na baadhi ya jamii yake, kuzuwiwa kuendesha darsa, kufungiwa misikiti asisalishe na mara kadhaa kupigwa mabomu ya machozi

(Endelea Katika Uk. 3)